TANGAZO LA SERIKALI NA. 363 la tarehe 10/05/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA VIWANDA MBEZI YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Viwanda Mbezi ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji
Sura ya 355

**2**. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji(mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango

**3**. Mipango kina katika eneo lililotajwa chini ya aya 2 itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba YD717 yenye majira - nukta 522685.565MS, 9257826.122KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.11 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IPC6

yenye majira – nukta 522790.116MS, 9257859.702KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.08 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba YY805 yenye majira - nukta 522815.736MS, 9257782.585KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.11 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba YZ47 yenye majira - nukta 522710.578MS, 9257752.101KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.08 hadi ulipoanzia"

Dodoma
25 April, 2024

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*